# JARIDA LA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

**Toleo la Mtandaoni: 05** | 07 Agosti, 2022 - TABORA | www.michezo.go.tz

# MABINGWA UMITASHUMTA 2022 WAANZA KUIBUKA



Wizara_SanaaTz

# MABINGWA UMITASHUMTA 2022 WAANZA KUIBUKA

## 07 Agosti, 2022



# Tabora na Manyara Zang'ara Katika Mchezo wa Kurusha Mkuki

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Timu ya wavulana Mkoa wa Tabora na timu ya Wasichana Mkoa wa Manyara zang'ara kwa kupata medali katika mchezo wa kurusha mkuki kwenye mashindano ya Michezo kwa Shule za Msingi (UMITASHUMTA) mwaka 2022 yanayoendelea Mkoani Tabora Agosti 07, 2022.

Katika mchezo huo kwa Wavulana, mwanafunzi Masesa Juma kutoka Tabora ameibuka kidedea kwa kurusha mkuki umbali wa mita 43.00, akifutiwa na Eliasi Kasale wa Arusha aliyerusha mita 39.21. Mshindi wa tatu ni Danieli Yona kutoka Manyara ambaye amerusha mita 38.49.

Kwa upande wa Wasichana, Mwanafunzi Ester Motaja kutoka Mkoa wa Manyara alierusha mita 36.97 akifuatiwa na Antonia Tarimo naye wa Manyara alierusha umbali wa mita 29.15.

Nafasi ya tatu imechukuliwa na wenyeji Tabora kupitia mwanafunzi Mahawi Juma alierusha kwa mita 28.97.

Kocha wa Manyara Amiri Juma Laswa alieleza kuwa Mkoa huo mwaka huu umeshinda Medali nyingi ikiwemo mchezo wa Riadha Wasichana mita 1500, kuruka chini, kurusha mikuki huku wakitarajiwa kufanya vizuri katika michezo mingine.

Aidha, ametumia nafasi hiyo kueleza kuwa Mkoa wa Manyara wapo tayari kuhesabiwa Agosti 23, 2022 na watakaporejea nyumbani watazidi kuihamasisha jamii kushiriki zoezi hilo muhimu.

Bingwa wa kurusha mkuki kwa wavulana Masesa Juma kutoka Tabora ameshinda kwa umbali wa mrusho wa mita 43.00




um





Bingwa wa kurusha mkuki kwa wasichana Ester Motaja kutoka Manyara ameshinda kwa umbali wa mrusho wa mita mita 36.97.










# Njombe Bingwa Soka Kundi Maalumu Wavulana

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Timu ya Mpira wa Miguu wavulana kundi maalumu kutoka Mkoa wa Njombe, imefanikiwa kushinda ubingwa wa mashindano ya michezo kwa shule za msingi (UMTASHUMTA) yanayoendelea kitaifa Mkoani Tabora.

Katika mchezo fainali iliyochezwa Agosti 07, 2022 kwenye uwanja Shule ya sekondari wavulana Tabora, timu ya Njombe imechukua ubingwa wa UMITASHUMTA 2022 baada ya kuishinda Mtwara kwa mikwaju ya Penati.

Mchezo huo ulifikia hatua ya matuta baada ya muda wa kawaida kumalizika zikiwa zimetoshana nguvu kwa sare ya 0 – 0, na Njombe kushinda kwa penati 4 dhidi ya 2 za Mtwara.

Njombe ni Bingwa mtetezi wa mchezo w kwa UMITASHUMTA 2021, hivyo wamefanikiwa kuutetea ubingwa kwa kushinda mara ya pili mfulululizo.

Kocha wa kikosi cha Mtwara Shazili Nangulukuta, akizungumzia kupoteza mchezo huo amekiri amesema iliku-



wa ni fainali ngumu huku akiwasifu vijana wake kwa kuonesha mchezo mzuri tangu mwanzo wa mashindano

“Vijana wameondolewa kwa mikwaju ya penati katika mchezo wa fainali, wamepambana sana hadi kufikia hatua hii, mashindano ya mwaka huu yalikuwa magumu na tumekutana na bingwa mtetezi katika fainali” amesema kocha wa Mtwara.

Kwa upande wa Kocha wa Timu ya Mkoa wa Njombe Mwakabidi Joseph amesema alijua kuwa michezo dhidi ya Mtwara hautakuwa rahisi kutokana na uimara wao tangu wakati wa hatua za awali.

“Mchezo ulikuwa mgumu, Mtwara tulikuwa nao kwenye kundi D katika hatua za awali na walitufunga 3 – 2, tulijua hautakuwa mchezo mrahisi na tunashuku tumeshinda na kutetea ubingwa wetu” ameongeza Mwakabidi.

Raymond Ndaka ambaye ni mmoja wa wachezaji wa timu ya Mkoa wa Mtwara ambaye ameonesha uwezo wa hali ya juu katika UMITASHUMTA 2022, amesema wameridhika na matokeo waliyoyapata na wanajipanga kwa wakati mwingine.

Kapteni wa timu ya mkoa wa Njombe Isack Sanga, amesema walijiandaa vizuri kushindana na Mtwara na walikuwa wanawaheshimu wakati wote wa mchezo ndio maana waliweza kufika nao kipindi cha penati na kuibuka washindi.

Katika mchezo wa awali kuwania nafasi ya tatu timu ya mkoa wa Dar es salaam iliibuka na ushindi wa magoli 2 – 0 dhidi ya Iringa, mchezo ambao ulichezwa saa 4 Asubuhi kwenye uwanja B shule ya sekondari wavulana Tabora.

Magoli ya Dar es salaam yalifungwa na Bakari Hamza dakika ya 1 na Ally Hashim aliyehitimisha ushindi kwa goli la dakika ya 24.



# Katavi na Mbeya Mshindi wa Tatu Mpira wa Wavu

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mkoa wa Katavi umeshika nafasi ya tatu katika mchezo wa Wavu (Volleyball) baada ya kuibamiza Geita Seti 3 kwa 1 upande wa Wavulana, huku Mbeya upande wa Wasichana ikiishinda Dar es Salaam kwa Seti 3 dhidi ya 0.

Mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Tabora Wavulana, Agosti 07, 2022, vijana wameonesha uwezo na vipaji vya hali ya juu na uwezo wa kutosha.

Mechi ya awali ilikua ya Wasichana kati ya Mbeya na Dar es Salaam upande wa Wasichana huku upande wa Wavulana kati ya Geita na Katavi.

Fainali inatarajiwa kufanyika baadae ambapo upande wa Wasichana itakua ni kati ya Mwanza na Mtwara na upande wa Wavulana itakua ni baina ya Mwanza na Mbeya.










# Geita Bingwa Netiboli UTMITASHUMTA 2022

Na Shamim Nyaki – **WUSM**

Mkoa wa Geita umeibuka Bingwa katika mchezo wa Netboli kwenye Mashindano ya Kitaifa ya Michezo ya Shule za Msingi mwaka 2022 Tabora, baada ya kuichapa Songwe magoli 71 kwa 49.

Mchezo huo uliochezwa katika Uwanja wa Chuo Cha Uhazili mkoani hapo, ulikuwa na mchuano mkali kutoka kwa timu zote mbili.

Katika mchezo huo, Mkoa wa Geita umemtumia nafasi zote walizopata walipokua na mpira dhidi ya wapinzani wao Mkoa wa Songwe.

Awali kabla ya mchezo wa mabingwa hao ilichezwa mechi kati ya Mkoa wa Mwanza na Mara ambapo Mkoa wa Mwanza mabingwa watetezi wameshinda nafasi ya tatu.

Mashindano hayo yatafika tamati Agosti 08, 2022.


WD
WA
C
GD
GS
GK


WD
GA
GK


WA
WA
WD
C
C



# Mwanza Waibuka Mabingwa wa Soka la Wasichana UMITASHUMTA

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Timu ya Mpira wa Miguu Wasichana kutoka Mkoa wa Mwanza, imefanikiwa kushinda ubingwa wa mashindano ya michezo kwa shule za msingi (UMTASHUMTA) yanayoendelea kitaifa Mkoani Tabora baada ya kuifunga Mara magoli 2 – 1.

Mchezo huo wa fainali umechezwa Agosti 07, 2022 saa 11:00 Jioni kwenye uwanja wa Shule ya Wavulana Tabora.

Mara ndio walikuwa wa kwanza kupata goli lililofungwa dakika ya 15 na Vanesa Paskali na kudumu kwa muda wa dakika 5 tu kabla ya Suzana Fabiana kusawazisha dakika ya 20.

Dakika ya 26 Fabiana kusawazisha alirudi tena nyavuni akifunga goli la 2 kwa mkaju wa penati, matokeo yaliyodumu hadi dakika ya mwisho na kuwapa Mwanza ubingwa wa UMITASHUMTA 2022.

Mchezo huo wa fainali umehitimisha michezo ya soka wasichana kwenye UMITASHUMTA 2022, inayotarajiwa kuhitimisha Agosti 8, 2022.



# Tabora, Dar Kuchuana Fainali UMITASHUMTA Wavulana

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Timu za mpira wa Miguu wavulana kutoka mikoa ya Tabora na Dar es salaam zimeingia fainali ya mashindano ya UMITASHUMTA 2022, baada ya kushinda michezo ya nusu fainali iliyochezwa Agosti 07, 2022.

Mchezo wa kwanza wa nusu fainali uliwakutanisha wenyeji Tabora na Rukwa katika mchezo uliofanyika uwanja A wa shule ya Sekondari wavulana Tabora.

Katika mchezo huo Tabora waliibuka washindi kwa goli 1 – 0 hivyo kutangulia fainali itakayochezwa Agost 08, 2022 saa 3:30 Asubuhi kwenye uwanja A shule ya sekondari wavulana Tabora.

Katika mchezo wa pili, Dar es salaam ilifanikiwa kuingia hatua ya fainali baada ya kuifunga Geita kwa magoli 2 – 0.

Dar es Salaam walikuwa wa kwanza kufunga goli dakika ya 5 kupitia Seleman Rashid ambalo lilisawazishwa dakika ya 42 na Tegemea Kapela, lakini baadae dakika ya 51 Jabir Abdallah akaihakikishia ushindi Dar es salaam baada ya kuongeza goli la pili na la mwisho.

Kufuatia matokeo hayo, wenyeji wa mashindano Tabora watakutana na Dar es salaam kwenye fainali ya soka kwa wvulana, mchezo abao unatarajiwa kuwa wa kuvutia.

Mchezo wa awali wa kumtafuta mshindi wa tatu utazikutanisha Rukwa na Geita majira ya saa 2:00 asubuhi kabla ya kushuhudia mchezo wa fainali utakaohitimisha rasmi mashindano ya UMITASHUMTA 2022.



# Mwanza na Mtwara Mabingwa Mpira wa Wavu

Na Bryson Mshana – **TABORA**

Mkoa wa Mwanza umenyakua kombe la Mpira wa Wavu upande wa Wavulana baada ya kuishinda Mbeya Kwa seti 3 kwa Moja, huku Mkoa wa Mtwara ukiibuka kidedea katika Upande wa Wasichana baada ya kuifunga Mwanza Seti 3 dhidi ya 2.

Mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Tabora Wavulana, Agosti 07, 2022, ilikuwa ya kuvutia n yenye upinzani mkali huku timu zote zikitumia nafasi za kutafuta ushindi kwa stadi.

Katika Mashindano hayo Mkoa wa Mwanza umefanikiwa kuingia fainali kwa timu zote mbili za Wasichana na Wavulana, hivyo kuwa miongoni mwa mikoa iliyoshika nafasi nyingi za juu kwenye michezo mbalimbali.

Mechi ya awali ilikua ya Wasichana kati ya Mbeya na Dar es Salaam upande wa Wasichana huku upande wa Wavulana kati ya Geita na Katavi.

Aidha, Mkoa wa Mbeya umefanikiwa kushika nafasi ya tatu upande wa Wasichana, huku Katavi ikiibuka nafasi hiyo upande wa Wavulana.


# SANA ZA UBUNIFU

Wanafunzi wanaoshiriki Michezo ya Shule za Msingi (UMITASHUMTA) mkoani Tabora, wameendelea kuonesha uwezo, na vipaji walivyonavyo katika fani mbalimbali.

Agosti 07, 2022 Wanafunzi wametengeneza vitu mbalimbali kutokana na malighafi zinazowazunguka katika mabweni waliyofikia.




TASAF II
BWAWA LA SAMAKI
LA
UNYANYEMBE
MRADI WA SAMAKI
NA AKINAMAMA
WAJANE
KIJIJI CHA UNYANYEMBE
TABORA
UZINDUZI WA
BWAWA LA SAMAKI
MRADI WA BWAWA LA
SAMAKI UMEZINDULIWA
LEO TAREHE 07'08'2022
NA MKURUGENZI WA
TASAF BI MADAM VIDA






GENGE




DRAFT
ALA ZA MUZIKI
MANYANGA
BAO

# UMITASHUMTA | UMISSETA
# 2022

# #SensaBika

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

www.michezo.go.tz